JAMHURI YA KENYA

**WIZARA YA MAZINGIRA, MABADILIKO YA HALI YA HEWA, NA MISITU**

**IDARA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA**


Dagoretti Corner, Ngong Road, SLP 30259, 00100 GPO, Nairobi, Kenya

**Simu:** 254 (0) 20 3867880-7, 0724 255 153/4

**Barua pepe:** director@meteo.go.ke, info@meteo.go.ke

**Twita:** @MeteoKenya



**Nambari ya kumbukumbu: KMD/FCST/6-2025/SO/02**

**Tarehe:03/09/2025**


## 1. TAARIFA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA KWA MSIMU WA VULI; OKTOBA –DISEMBA 2025

Msimu wa mvua za vuli (Oktoba-Novemba-Disemba, OND) ni wa umuhimu mkubwa nchini Kenya, hasa kwa maeneo ya kati na mashariki ya nchi.

**Dondoo muhimu za msimu wa mvua za Vuli kipindi cha Oktoba – Disemba, 2025**

Tathmini ya hali ya hewa kwenye msimu huu wa mvua za vuli "Oktoba–Desemba 2025" inaonyesha kuwa sehemu kubwa ya Kaskazini Mashariki, maeneo ya chini ya Kusini Mashariki na ukanda wa Pwani yanatarajiwa kupokea mvua kiwango cha chini ya wastani.

Kusini ya Bonde la Ufa, maeneo ya Kati, sehemu kubwa ya eneo la Ziwa Viktoria, baadhi ya sehemu za Nyanda za juu ya Mashariki ya Bonde la Ufa ikiwemo Kaunti ya Nairobi, maeneo machache katika sehemu za chini ya Kusini Mashariki (baadhi ya sehemu za Kajiado) na sehemu za magharibi ya kaunti ya Samburu na Marsabit yanatarajiwa kupokea kiwango cha mvua cha karibu na wastani hadi chini ya wastani. Nyanda za juu Magharibi ya Bonde la Ufa na baadhi ya maeneo ya Kaskazini Magharibi yanatarajiwa kupokea kiwango cha mvua cha karibu na wastani hadi zaidi ya wastani.

Hali hii inachochewa na hali inayoendelea ya "*Indian Ocean Dipole*" (IOD) hasi (-), ambayo ndio kichocheo kikuu cha utabiri huu, IOD hasi inatarajiwa kuendelea kuanzia mwezi wa Septemba hadi Novemba 2025 kabla ya kurejea katika hali ya kawaida kufikia mwezi wa Disemba. IOD hasi kwa kawaida huleta hali ya ukame kuliko kawaida katika Ukanda wa Afrika Mashariki, kwa hivyo kuweza kupunguza mvua za msimu wa vuli.

Kulingana na taarifa iliyotolewa tarehe 2 Septemba 2025 na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), kuna uwezekano wa takribani asilimia 55 wa kutokea kwa "*La nina*" katika kipindi cha Septemba–Novemba 2025, uwezekano huo unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 60 katika kipindi cha Oktoba–Desemba 2025, kadhalika, uwezekano wa "*El nino*" unazingatiwa kuwa wa kiwango cha chini sana. Idara ya Hali ya Hewa ya Kenya (KMD) itaendelea kutathmini kwa ukaribu sana hali ya vichocheo hivi "ENSO".

Mgao wa mvua unatarajiwa kuwa wa duni katika sehemu nyingi nchini, ukiambatana na vipindi virefu vya ukame, pia, vipindi vichache vya dhoruba za mara kwa mara vinatarajiwa.

## 2.0 Utabiri wa kina katika Msimu wa Vuli (Oktoba-Disemba) 2024 ni kama ifuatavyo*:*

**2.1 Kaunti za nyanda za juu Magharibi ya Bonde la Ufa (Kisii, Nyamira, Trans Nzoia, Uasin Gishu, West Pokot, Elgeyo Marakwet, Nandi, Kericho, Bomet, Kakamega, Vihiga, Bungoma na sehemu za magharibi ya Baringo):** Mvua inayotarajiwa msimu huu ni ya karibu na wastani hadi juu ya wastani. Mgao wa mvua hizi unatarajiwa kuwa wa wastani hadi wa kuridisha, huku dhoruba za hapa na pale zikitarajiwa kutokea.

**2.2 Bonde la Ziwa Viktoria (Kaunti za Siaya, Kisumu, Homa Bay, Migori na sehemu za kusini ya Busia):** Mvua inayotarajiwa ni ya karibu na wastani hadi chini ya wastani, isipokuwa katika sehemu za kaskazini ya Busia ambamo mvua ya karibu na wastani hadi zaidi ya wastani inatarajiwa. Usambazaji wa mvua unatarajiwa kuwa duni hadi wa wastani, huku dhoruba za mara kwa mara zikitarajiwa.

**2.3 Maeneo ya Kati na Kusini ya Bonde la Ufa (Kaunti za Nakuru, Narok na sehemu za Baringo):** Mvua inayotarajiwa ni ya karibu na wastani hadi chini kidogo ya wastani. Mgao wa mvua hizi unatarajiwa kuwa duni hadi wa wastani, huku dhoruba za hapa na pale zikitarajiwa.

**2.4 Kaskazini Magharibi (Kaunti ya Turkana):** Maeneo haya yanatarajiwa kupokea mvua za hapa na pale ambazo zitakuwa za karibu na wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hata hivyo, vipindi virefu vya ukame vinatarajiwa. Mgao wa mvua hizi unatarajiwa kuwa duni.

**2.5 Kaskazini Magharibi (Kaunti ya Samburu):** Maeneo haya yanatarajiwa kupokea mvua za mara kwa mara ambazo zitakuwa za karibu na wastani mpaka chini kidogo ya wastani katika sehemu za magharibi ya Samburu, na chini ya wastani katika maeneo mengine ya kaunti. Vipindi virefu vya ukame vinatarajiwa, na mgao wa mvua hizi unatarajiwa kuwa wa kutoridhisha.

**2.6 Nyanda za juu Mashariki ya Bonde la Ufa (ikiwemo eneo la Nairobi): (Nairobi, Nyeri, Kirinyaga, Murang'a, Kiambu, Meru, Nyandarua, Embu, Tharaka Nithi)** Kaunti hizi zinatarajiwa kupata mvua za msimu utakaokumbwa na vipindi vya ukame. Jumla ya kiasi cha mvua kinatarajiwa kuwa cha karibu na wastani hadi chini ya wastani katika maeneo ya Nairobi, Kiambu, Nyandarua, sehemu za Murang'a na Nyeri, na chini ya wastani katika maeneo yaliyosalia. Usambazaji wa mvua unatarajiwa kuwa duni hadi wa wastani kwa muda na wakati, Zaidi ya hayo, dhoruba za mara kwa mara zinaweza zikashuhudiwa.

**2.7 Maeneo ya Chini ya Kusini Mashariki (Kaunti za Kitui, Makueni, Taita Taveta, Kusini Mashariki ya Kajiado, Tana River na sehemu za kati na mashariki ya Machakos):** Kaunti hizi zinatarajiwa kupata mvua za hapa na pale. Mvua hii inatarajiwa kuwa ya chini ya wastani. Vipindi virefu vya ukame pia vinatarajiwa, aidha, mgao wake unatarajiwa kuwa duni.

**2.8 Kaunti za Kaskazini Mashariki (Mandera, Wajir, Garissa, Isiolo na sehemu za mashariki za Marsabit):** Maeneo haya yanatarajiwa kupata mvua za hapa na pale katika msimu huu. Hata hivyo, jumla ya kiasi cha mvua kinatarajiwa kuwa chini ya wastani. Vipindi virefu vya ukame pia vinatarajiwa, huku mgao wake ukitarajiwa kuwa wa kutoridisha.

**2.7 Kaunti za Pwani (Mombasa, Kilifi, Lamu, Kwale na maeneo ya Pwani ya Tana River):** Kaunti hizi zinatarajiwa kupata mvua za awamu. Zaidi ya hayo, kiwango cha mvua hizi kinatarajiwa kuwa cha chini ya wastani. Vipindi virefu vya ukame na dhoruba za hapa na pale pia vinatarajiwa, isitoshe mgao wake ni duni.

## 3.0 TAARIFA YA MGAO WA MVUA ZA VULI 2025, TAREHE ZA YANZO NA KIKOMO CHA MSIMU.

Utabiri wa tarehe za yanzo, kikomo na mgao wa mvua za vuli umetokana na uchambuzi wa twakimu za yaka uliopita (2021), ambao ulikuwa na dhalili sawia na za yaka huu. Mgao wa mvua hizi za vuli unatarajiwa kuwa wa wastani hadi mzuri kwenye maeneo ya magharibi, ilhali maeneo ya kati yanatarajiwa kupata mgao duni hadi wa kuridisha. Maeneo yaliyosalia yanatarajiwa kupata mgao duni wa mvua hizi.

### 3.1 TAREHE ZA MIANZO NA KIKOMO CHA MVUA ZA VULI 2025

Tarehe za mianzo na kikomo kwa mvua za vuli kuendana na Kaunti ni kama ifuatavyo:

| **Sehemu** | **Mianzo** | **Kikomo** | **Mgao kwa wakati na nafasi** |
|---|---|---|---|
| **Kaunti za Magharibi** (Busia, Vihiga, Kakamega, Bungoma); **Kaunti za Nyanza** (Kisumu, Siaya, Homa Bay, Nyamira, Migori, Kisii);na **Kaunti za Bonde la Ufa** (Kericho, West Pokot, Nandi, Bomet, Uasin Gishu, Trans Nzoia, Nakuru, Elgeyo Marakwet, Baringo). | Mvua itaendelea tokea mwezi wa Septemba | Wiki ya tatu hadi nne ya Disemba | Wastani mpaka mzuri |
| **Kaunti za Kati ya Kenya** (Kirinyaga, Nyeri, Murang'a, Nyandarua, Laikipia, Kiambu, Meru, Embu, Tharaka Nithi); Nairobi. | Wiki ya tatu hadi nne ya Oktoba | Wiki ya tatu hadi nne ya Disemba | Duni hadi ya wastani |
| **Kaunti za Kaskazini Magharibi** (Turkana, Samburu) | Haijabainika wazi, lakini mvua za hapa na pale zinatarajiwa kuendelea tokea mwezi wa Septemba | Hakijabainika | Duni |
| **Ukanda wa Pwani** (Kwale, Mombasa, Kilifi, Lamu, na sehemu ya pwani ya Tana River) | Wiki ya tatu hadi nne ya Novemba ila kuna uwezeakano wa mvua za hapa na pale Oktoba | Wiki ya tatu hadi ya nne ya Disemba | Duni |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Kusini ya Bonde la Ufa** (Narok) | Wiki ya nne ya Oktoba hadi ya kwanza Novemba ila kuna uwezeakano wa mvua za hapa na pale kutokea Septemba | Mvua itaendelea mpaka mwezi wa kwanza, 2026 | Duni mpaka wastani |
| **Kaunti za Kaskazini Mashariki** (Mandera, Wajir, Garissa, Marsabit, Isiolo) | Haujabainika | Hakijabainika | Duni |
| **Kaunti za Kusini-Mashariki** (Machakos, Makueni, Kitui, Taita Taveta, Kajiado, Tana River) | Wiki ya tatu hadi nne ya Novemba. | Wiki ya tatu hadi nne ya Disemba. | Duni |

**Kiambatanisho 1: Tarehe za Mianzo na kikomo cha mvua za vuli (Oktoba-Novemba-Disemba) 2025**

## 4. UTABIRI WA HALI YA UKAME NCHINI

Utabiri wa kiashiria cha hali ya ukame (drought index; SPI) unaonyesha kuongezeka kwa hatari ya kupata mvua chini ya wastani katika sehemu nyingi nchini. Uwezekano wa hali ya ukame wa kiwango cha chini (SPI < -0.09) umetabiriwa kuwa kati ya asilimia 55–90 ikilinganishwa na hali ya kawaida ya kiasili ya asilimia 46, huku hatari kubwa zaidi ikiwa katika maeneo ya mashariki na ya kati. Uwezekano wa kukolea kwa ukame (SPI < -0.98) pia umeongezeka hadi kati ya asilimia 20–55 ikilinganishwa na asilimia ya kawaida ya 16, hasa katika maeneo ya mashariki. Utabiri huu unaashiria kwamba maeneo mengi huenda yakaingia katika hatua ya ukame wa kiwango cha chini (tahadhari), huku kukiwa na uwezekano mkubwa wa kuzidi na kufikia hatua ya ukame mkali (hatari) kadri msimu unavyoendelea.

## 5. MTAZAMO WA HALI YA JOTO NCHINI

Utabiri wa halijoto unaonyesha kuwa maeneo mengi nchini yanatarajiwa kuwa na joto la juu ya wastani, isipokuwa maeneo machache katika eneo la magharibi ambapo joto linatarajiwa kuwa la karibu na wastani hadi chini ya wastani. Uwezekano mkubwa wa joto kuwa juu ya wastani unatabiriwa katika maeneo ya katikati na mashariki ya nchi.

## 6. ATHARI ZINAZOTARAJIWA KUTOKANA NA MVUA ZA VULI 2025

Mvua zinazotarajiwa katika msimu wa Oktoba hadi Desemba zinatarajiwa kuwa na athari chanya na hasi katika sekta mbalimbali. Athari kuu ambazo huenda zikajitokeza kutoka na vua hizi za vuli zitatolewa na wadau wa sekta husika.

***Kumbuka: Kuna vichocheo vya katikati ya msimu vinavyosababisha mabadiliko ya hali ya hewa, kama vile vimbunga vya kitropiki na mzunguko wa Madden-Julian (MJO), ambavyo vinaweza kutabirika tu kwa muda mfupi kabla. Hivyo basi, ni muhimu kufuatilia utabiri na taarifa zinazotolewa mara kwa mara na idara hii. Vilevile, utabiri huu wa mvua za vuli utumike pamoja na tabiri za hali ya hewa za siku 5, za wiki, mwezi zikifuatanishwa na jumbe fupi boresha, ripoti za ushauri +-na jumbe za athari pamoja na tabiri za wiki na mwezi za Kaunti tokea Ofisi za huduma ya hali ya hewa katika kila Kaunti nchini.***

Charles Mugah

**KWA NIABA YA: MKURUGENZI WA IDARA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA NCHINI KENYA.**